

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**BUNGE LA TANZANIA**



**ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO**

**MKUTANO WA TATU**

**KIKAO CHA HAMSINI NA TISA**

**25 JUNI, 2021**



## ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

### MKUTANO WA TATU

KIKAO CHA HAMSINI NA TISA – TAREHE 25 JUNI, 2021

I. DUA:

II. MASWALI:

OFISI YA RAIS (TAMISEMI):

490. **MHESHIMIWA ASKOFU JOSEPHAT  
MATHIAS GWAJIMA (KAWE):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, Serikali haioni kuwa ni wakati muafaka wa kuzipandisha hadhi Barabara za ndani za Jimbo la Kawe ili zihudumiwe na TANROADS kwa kuwa uwezo wa TARURA ni kuhudumia Km 120 wakati Jimbo lina barabara zenye jumla ya Km 1463.

**491. MHESHIMIWA JOSEPH MICHAEL MKUNDI (UKEREWE):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, ni lini Mamlaka ya Mji Mdogo Nansio itatambuliwa rasmi na kuanza kuwahudumia Wananchi.

**WIZARA YA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO:**

**492. MHESHIMIWA SHAMSIA AZIZI MTAMBA (MTWARA VIJIJINI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Afya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto:-

Je, ni lini Serikali itawapatia Wazee hasa wa Vijijini Bima ya Afya ikiwemo ya CHF inayotolewa na Halmashauri.

**WIZARA YA UJENZI NA UCHUKUZI:**

**493. MHESHIMIWA ENG. MWANAISHA NG'ANZI ULENGE (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi:-

Je, ni lini ahadi ya upanuzi wa Uwanja wa Ndege Tanga iliyotolewa na Mheshimiwa Rais wakati wa Uzinduzi wa Mradi wa Bomba la Mafuta pale Chongoleani itaanza kutekelezwa.

**494. MHESHIMIWA MRISHO MASHAKA GAMBO (ARUSHA MJINI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi:- Jimbo la Arusha Mjini limekuwa likisumbuliwa na changamoto ya mafuriko kwenye Kata za Sombetini, Levolosu, Osunyai, Seki, Unga LTD, Sakina, Baraa na Olorien yanayosabishwa na Miundombinu mibovu ya Barabara ya Sakina – Tengeru - Airport na Soko la Kilombero:-

Je, ni lini Serikali itatengeneza Miundombinu hii ili kuwaondolea Wananchi adha hiyo.

**WIZARA YA NISHATI:**

**495. MHESHIMIWA AYSHAROSE NDOGHOLI MATTEMBE (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nishati:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kupeleka umeme katika Vijiji 14 vya Jimbo la Manyoni Magharibi.

## **WIZARA YA KILIMO:**

**496. MHESHIMIWA SHALLY JOSEPHA  
RAYMOND (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Kilimo:-

Je, ni lini makubaliano ya kibiashara yatafanyika baina ya Taasisi za Umma na Makampuni binafsi yanayolima Kahawa Mkoani Kilimanjaro ili kuzalisha miche bora yenye ukinzani dhidi ya magonjwa na kuigawa kwa Wakulima bila malipo.

## **WIZARA YA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI:**

**497. MHESHIMIWA ENG. STELLA MARTIN  
MANYANYA (NYASA):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki:

Je, Serikali ina mpango gani wa kuimarisha Biashara kupitia Diplomasia ya Uchumi kati ya Tanzania na Malawi kwa kutumia Meli ya MV Mbeya II.

## **WIZARA YA FEDHA NA MIPANGO:**

### **498. MHESHIMIWA JULIANA DANIEL SHONZA (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Mipango:-

Je, Serikali imejipangaje kutatua changamoto ya msongamano wa magari yanayovuka kuelekea Nchi jirani kupitia Mpaka wa Tunduma.

### **III. UCHAGUZI WA WAJUMBE KWENYE TAASISI MBALIMBALI:**

1. Tume ya Utumishi wa Bunge;
2. Bunge la Afrika (*PAP*);
3. Jukwaa la Wabunge wa Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika (*SADC – PF*);
4. Umoja wa Wabunge Duniani (*IPU*); na
5. Umoja wa Maziwa Makuu (*Great Lakes*).

**DODOMA  
25 JUNI, 2021**

**N.J. MWIHAMBI, *ndc*  
KATIBU WA BUNG**